TANGAZO LA SERIKALI NA. 913 la tarehe 22/12/2023

SHERIA YA FEDHA YA SERIKALI ZA MITAA,

(SURA YA 290)

# SHERIA NDOGO

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 7(1) na 16(1))*

SHERIA NDOGO YA ADA NA USHURU YA HALMASHAURI YA WILAYA YA KOROGWE YA MWAKA 2023

Jina

1. Sheria Ndogo hii itajulikana kama Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe ya Mwaka 2023.

Matumizi

2. Sheria Ndogo hii itatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe.

Tafsiri

3. Katika Sheria Ndogo hii, isipokuwa kama muktadha utahitaji vinginevyo-

"ada" maana yake ni malipo yanayolipwa kwa Halmashauri kwa ajili ya vibali au leseni mbalimbali zitolewazo na Halmashauri;

"ada ya ardhi" maana yake ni ada itakayotozwa kutokana na huduma za matumizi ya uendelezaji wa ardhi na upimaji;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni afisa yeyote aliyeteuliwa na Mkurugenzi kwa lengo la kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hii;

"chombo cha usafiri" maana yake ni chombo cha moto au chombo chochote kinachotumika kusafirishia bidhaa, abiria au mizigo;

"Halmashauri" maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya

Korogwe;

"hifadhi ya barabara" maana yake ni kama ilivyotafsiriwa katika Sheria ya Barabara;

"kibali" maana yake ni idhini ya maandishi inayotolewa na Halmashauri kwa mujibu Sheria Ndogo hii;

"kibali cha burudani" maana yake ni kibali cha maandishi kinachotolewa na Halmashauri kwa ajili ya kufanya shughuli za burudani ambayo inakutanisha watu katika ukumbi, uwanja wa michezo au sehemu yoyote ya wazi au mitaani;

"kibanda" maana yake ni jengo au chumba cha biashara;

"kupiga debe" maana yake ni kushawishi abiria kusafiri kwa kutumia chombo fulani cha usafiri kwa kumshika au kumsongasonga au kushika mzigo wa abiria;

"machinjio" maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinjia wanyama na kuanika ngozi;

"madini ya ujenzi" maana yake ni tarazo, moramu, udongo, kifusi, kokoto, mawe, mchanga, chokaa na madini mengine yanayotumika katika ujenzi;

"mazao ya majini" maana yake ni samaki, dagaa, magamba ya samaki, na vitu vyote vyenye asili ya samaki;

"meza au kizimba" maana yake ni kitu au kifaa kinachotumika kuweka bidhaa kwa ajili ya kuuza sokoni au gulioni;

"mhudumu" maana yake ni mtu yeyote anayehudumia wateja katika eneo la biashara;

"Mkurugenzi" maana yake ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe au afisa yeyote aliyeteuliwa kutekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

"mnada" maana yake soko la wazi ambalo mali au vitu mbalimbali vinauzwa kwa ushindani wa bei kwa kauli na kwa kibali maalumu cha Halmashauri;

"mnara wa mawasiliano" maana yake ni mnara uliowekwa kwa ajili ya kuwezesha mawasilino ya simu, redio au televisheni ndani ya eneo la Halmashauri;

"soko" maana yake ni eneo au soko liliotengwa na linalomikiwa na Halmashauri kama soko;

"stendi" maana yake ni eneo maalum lililotengwa au kujengwa na Halmashauri kwa ajili ya kupakia na kushusha abiria au mizigo;

"ushuru" maana yake ni maana yake ni tozo inayotozwa na Halmashauri kwa shughuli au huduma mbalimbali zinazofanywa katika eneo la Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni kampuni iliyoteuliwa kukusanya ushuru kwa niaba ya Halmashauri chini ya Sheria Ndogo hii.

Sura ya 167

Utozaji wa ada au ushuru

4.-(1) Halmashauri itatoza ada au ushuru kwa ajili ya vibali, leseni na huduma mbalimbali zinazotolewa na Halmashauri kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la Kwanza la Sheria Ndogo hii.

(2) Kwa kuzingatia masharti ya aya ndogo ya (1), ada au ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hii utalipwa kwa Halmashauri au wakala wa Halmashauri kwa kadri Halmashauri itakavyoelekeza.

(3) Malipo ya ada au ushuru yatalipwa kabla au wakati wa kupokea huduma inayotozwa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii.

Wajibu wa kulipa ada au ushuru

5. Mtu yeyote anayestahili kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii atatakiwa kulipa ada au ushuru huo kwa kuzingatia viwango vilivyoainishwa katika Sheria Ndogo hii.

Ukusanyaji wa ada au ushuru

6.-(1) Muda wa kukusanya ada au ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili kamili asubuhi hadi saa kumi na mbili kamili jioni.

(2) Bila kujali masharti ya aya ndogo ya (1), Halmashauri au wakala, kwa kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ada au ushuru baada ya muda ulioainishwa kwenye aya hii..

(3) Malipo ya ada na ushuru yatafanyika kila siku au kwa mwezi au kwa namna yeyote itakayokubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa ada au ushuru.

(4) Endapo mlipaji atakamilisha malipo yaliyoainishwa kwenye Sheria Ndogo hii, atapaswa kupewa stakabadhi ya kielektroniki ya Halmashauri kama kielelezo cha malipo yaliyofanyika.

Ukusanyaji wa madeni

7. Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ada au ushuru kwa njia ya Mahakama endapo mtu au taasisi itakuwa imeshindwa kulipa kwa muda uliokubaliwa.

(2) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (1), Halmashauri inaweza kukusanya madeni ya ushuru kwa njia ya kukamata au kushikilia mali zinazohamishika za wadaiwa zenye thamani sawa na deni la ushuru pamoja na gharama za kukamata.

(3) Baada ya kipindi cha siku thelathini kupita tangu kukamatwa kwa mali za mdaiwa, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuziuza kwa njia ya mnada baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(4) Endapo mali zilizokamatwa zinaweza kuharibika kwa haraka, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuziuza kabla hazijaharibika baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(5) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (3) na (4), kabla ya Halmashauri kuuza mali yoyote iliyokamatwa, Mkurugenzi atatoa taarifa ya siku saba kwa mdaiwa na umma juu ya kusudio la kuuza mali hizo.

(6) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote itakayotokea wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayokamatwa na kushikiliwa na Halmashauri, isipokuwa kama hasara hiyo itakuwa imesababishwa na uzembe wa watumishi wa Halmashauri au wakala.

Uteuzi wa Wakala

8.-(1) Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuteua wakala watu kwa ajili ya kukusanya ushuru au ada kwa niaba

yake kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

(2) Wakala aliyeteuliwa kwa mujibu wa aya ndogo ya (1) atakuwa na wajibu wa:

(a) kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba wa uwakala alioingia na Halmashauri;

(b) kukusanya ushuru kwa kutumia mfumo wa kielektroniki.

Makosa ya Wakala

9. Wakala aliyeteuliwa na Halmashauri atakuwa ametenda kosa endapo:

(b) atajaribu au atakusanya ada na ushuru kwa kiwango tofauti na kilichoainishwa katika Sheria Ndogo hii;

(c) atashindwa kuwasilisha au atawasilisha pungufu ya kiwango cha ada na ushuru kilichokubaliwa katika mkataba;

(d) atakusanya ada na ushuru kwa taratibu tofauti na alizoelekezwa na Halmashauri; na

(e) hatazingatia maelekezo yoyote muhimu atakayopewa na Halmashauri wakati wa kutekeleza majukumu yake.

Maeneo ya machinjio

10. Mtu yeyote anayetaka au atakayetaka kuchinja wanyama atatakiwa kuchinja wanyama wake kwenye machinjio yatakayoainishwa na Halmashauri.

Mamlaka ya Afisa Mwidhiniwa

11. Bila kuathiri masharti mengine ya Sheria Ndogo hii, Afisa Mwidhiniwa anaweza kuingia katika eneo, jengo au chombo cha usafiri wakati wa muda wa kazi kwa nia ya kukusanya ada au ushuru, kufanya tathmini au kufanya jambo lolote linalohusu ada, ushuru, leseni au kibali kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii.

Minara ya mawasiliano

12.-(1) Mtu yeyote anayekusudia kujenga mnara wa mawasiliano atatakiwa kuomba kibali cha maandishi kutoka

Halmashauri.

(2) Endapo mtu atajenga mnara wa mawasiliano bila kibali, Halmashauri itatoa Notisi ya siku saba ya kumtaka mtu huyo kuondoa mnara huo.

(3) Bila kuathiri masharti ya aya ndogo ya (2), mtu atakayepewa notisi ya kuondoa mnara atatakiwa kuondoa mnara huo kwa gharama zake binafsi, na endapo atashindwa kuondoa mnara huo Halmashauri itauondoa na atatakiwa kuilipa Halmashauri gharama iliyotumika.

Makosa na adhabu

13.-(1) Mtu yeyote atakuwa ametenda kosa endapo:

(a) atashindwa kulipa ada au ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii;
(b) atamshawishi mtu au kundi la watu kukwepa au kukataa kulipa ada au ushuru;
(c) atamzuia Mkurugenzi, Afisa Mwidhiniwa au Wakala kutekeleza majukumu yake chini ya Sheria Ndogo hii;
(d) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au Wakala kuhusu shughuli zinazohitaji kulipiwa ada au ushuru;
(e) atashindwa kuweka kumbukumbu, vitabu, hesabu au maelezo yoyote yatakayohitajika na Halmashauri;
(f) atashindwa, atadharau, atakaidi au kukataa kulipa ada au ushuru au atakataa kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kuhusiana na ulipaji wa ada au ushuru chini ya Sheria Ndogo hii; na
(g) atatengeneza, atatayarisha, ataidhinisha kutengeneza au atatunza nyaraka za uongo kwa nia ya kujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa ada au ushuru ndani ya Halmashauri.

Kufifilisha

14. Mkurugenzi atakuwa na uwezo wa kufifilisha kosa

kosa

kwa kumtoza mtu yeyote aliyetenda kosa chini ya Sheria Ndogo hii kiasi cha shilingi laki mbili endapo mkosaji atakiri kosa na kuwa tayari kujaza fomu maalum iliyoainishwa katika Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hii na kulipa ada au ushuru anaodaiwa.

Kufutwa kwa Sheria Ndogo TS Na. 71, 72, 74 na 73 ya mwaka 2011 na TS Na. 556 na 557 ya mwaka 2015

15. Sheria Ndogo ya (Ada na Ushuru) ya Halmashauri ya Wilaya Korogwe ya mwaka 2011; Sheria Ndogo ya (Ushuru wa Mazao) ya Halmashauri ya Wilaya Korogwe ya mwaka 2011; Sheria Ndogo ya (Ushuru wa Madini ya Ujenzi) ya Halmashauri ya Wilaya Korogwe ya mwaka 2011; Sheria Ndogo ya (Ushuru wa Stendi) ya Halmashauri ya Wilaya Korogwe ya mwaka 2011; Marekebisho ya Sheria Ndogo ya (Ushuru wa Mazao) ya Halmashauri ya Wilaya Korogwe ya mwaka 2015 na (Marebisho) ya Sheria Ndogo ya (Ushuru Madini ya Ujenzi) ya Halmashauri ya Wilaya Korogwe ya mwaka 2015, zinafutwa.

---

## JEDWALI LA KWANZA

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 4(1))*

### SEHEMU YA KWANZA: ADA YA KIBALI CHA UJENZI

| Namba | Aina ya Mchoro | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1 | Majengo yote ya nyumba za makazi | 300/= kwa kila mita ya mraba |
| 2 | Majengo yote ya biashara | 500/= kwa kila mita ya mraba |
| 3 | Majengo yote ya makazi na biashara | 500/= kwa kila mita ya mraba |
| 4 | Uzio wa mipaka (jengo la Makazi) | 500/= kwa kila mita |
| 5 | Uzio wa mipaka (jengo la biashara) | 600/= kwa kila mita |
| 6 | Uzio wa jengo la makazi na biashara | 600/= kwa kila mita |
| 7 | Endapo ni ghorofa kila ghorofa itahesabiwa ukubwa wa eneo lake | |

### SEHEMU YA PILI: ADA YA KIBALI CHA KUWEKA MATANKI

| Namba | Aina ya Matanki | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Matanki ya mafuta au gesi | 1,500 kwa kila mita moja ya ujazo |

*Tangazo La Serikali Na. 913 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 2. | Matanki ya Maji | 500 kwa kila mita moja ya ujazo |
| 3. | Matanki ya Maji ya viwandani au biashara | 500 kwa kila mita moja ya ujazo |
| 4. | Matanki ya maji | 150 kwa kila mita moja ya ujazo |

SEHEMU YA TATU: ADA YA MAOMBI YA KIBALI CHA KUWEKA MINARA YA MAWASILIANO

| Namba | Aina ya Huduma | Kiwango cha Ada ya Kibali (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Maombi ya ujenzi | 200,000/= |
| 2. | Maombi ya kuweka Mnara | 20,000 kwa kila mita ya mraba |

SEHEMU YA NNE: ADA YA UKARABATI WA JENGO NA KUZINGIRA WAKATI WA UJENZI

| Namba | Aina | Kiwango cha Ada ya Kibali (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ukarabati wa makazi | 50,000/= |
| 2. | Ukarabati wa hoteli au vituo vya mafuta au Taasisi na viwanda | 200,000/= |
| 3. | Ada kuzingira Makazi<br>Biashara na Makazi | 100,000= kwa mwaka<br>200,000/= kwa mwaka |

SEHEMU YA TANO: USHURU WA KUKODI MITAMBO/MALI ZA HALMASHAURI

| Nmba | Mtambo au Kifaa | Gharama (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Lori | 100,000/= kwa masaa 10 |
| 2. | Ukumbi | 200,000/= kwa masaa 8 |

SEHEMU YA SITA : USHURU WA BIDHAA ZA MISITU

| Namba. | Bidhaa | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Magogo ya miti mikubwa (kwa wenye vibali) | 5,000/= kila meta ya ujazo |
| 2. | Mbao za miti ya kupandwa | 3,500/= ya meta ya ujazo |
| 3. | Mbao za miti ya asili | 500 kwa ubao |

*Tangazo La Serikali Na. 913 (Linaendelea)*

| | | |
|---|---|---|
| 4. | Gunia la mkaa –Kubwa | 1,500/= kwa kila gunia |
| 5. | Gunia la mkaa –Dogo | 1,000/= kwa kila gunia |
| 6. | Nguzo za miti ya kupandwa | 150/= kwa kila nguzo |
| 7. | Nguzo za miti ya asili | 700/= kwa kila nguzo |
| 8. | Kuni | 1,000/= kwa mita za ujazo |
| 9. | Ada ya kutembelea maeneo ya vivutio na kupiga picha | Dola 5 ya Kimarekani kwa raia wa kigeni<br>Shilingi. 1,000/= wazawa |

SEHEMU YA SABA: USHURU WA MIFUGO

| Namba. | Mifugo | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Kununua mifugo mnadani | 4,000/= kwa ng'ombe na Punda<br>1000/= kwa mbuzi, nguruwe na kondoo |
| 2. | Ukaguzi wa nyama baada ya mnyama kuchinjwa | 3,000/= kwa ng'ombe<br>2,000/= kwa mbuzi, kondoo na nguruwe |
| 3. | Mifugo inayozurura | 50,000/= kwa kila ng'ombe<br>10,000/=kwa kila mbuzi, kondoo na nguruwe<br>50,000/= kwa kila punda |

SEHEMU YA NANE: USHURU WA MAZAO YA BIASHARA NA CHAKULA

| Namba | Mazao | Ujazo (KGS) | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| 1. | Mahindi | 100 | 2% ya bei ya shambani |
| 2. | Mpunga | 100 | 2% ya bei ya shambani |
| 3. | Mchele | 100 | 2% ya bei ya shambani |
| 4. | Mtama | 100 | 2% ya bei ya shambani |
| 5. | Ufuta | 100 | 3% ya bei ya shambani |
| 6. | Alizeti | 100 | 3% ya bei ya shambani |
| 7. | Pamba | 100 | 3% ya bei ya shambani |
| 8. | Korosho | 100 | 3% ya bei ya shambani |
| 9. | Maharage | 100 | 3% ya bei ya shambani |
| 10. | Kunde au Mbaazi au choroko | 100 | 3% ya bei ya shambani |
| 11. | Kahawa | 100 | 3% ya bei ya shambani |
| 12. | Tangawizi | kwa kilo | 3% ya bei ya shambani |
| 13. | Iliki | kwa kilo | 3% ya bei ya shambani |
| 14. | Kakao | 100 | 2,500.00 |
| 15. | Matunda yote | kwa gari fuso kubwa | 70,000.00 |

*Tangazo La Serikali Na. 913 (Linaendelea)*

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | (Tandamu) | |
| | | Kwa gari Fuso Dogo au kenta | 45,000.00 |
| | | Pickup | 20,000.00 |
| | | Gunia moja | 1,000.00 |
| 16. | Miwa | Kwa fuso | 40,000.00 |
| | | Kwa kenta | 20,000.00 |
| 17. | Mazao mengine ya chakula (asali, maziwa ) | Kwa lita | 2% ya bei ya shambani |
| 18. | Mazao mengine | 100 | 2,500/= |

SEHEMU YA TISA: ADA YA USAJILI WA VIKUNDI VYA KIJAMII NA VIKOBA

| Namba. | Maelezo | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya usajili ya vikundi vya kijamii | 40,000/= |
| 2. | Ada ya usajili wa vikoba | 40,000/= |

SEHEMU YA KUMI: ADA YA KUCHIMBA MADINI YA UJENZI

| Namba | Aina | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ada ya kibali cha kuchimba madini ya ujenzi | 200 kwa kila mita ya mraba |
| 2. | Mchanga | 1,000 kwa tani moja |
| 3. | Udongo au Kifusi | 1,000 kwa tani moja |
| 4. | Kokoto | 2,000 kwa tani moja |
| 5. | Mawe au Chokaa | 2,000 kwa tani moja |
| 6. | Rasilimali nyingine (Madini mengine) | 2,000 kwa tani moja |

SEHEMU YA KUMI NA MOJA: USHURU WA MADINI YA UJENZI KUTOKA KWENYE MAENEO MENGINE YASIYOMILIKIWA NA HALMASHAURI

| Namba. | Uzito wa Gari | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Tani 1 hadi 3 | 2,000/= kwa safari |
| 2. | Tani 4 hadi 7 | 3,000/= kwa safari |
| 3. | Tani 8 hadi 10 | 4,000/= kwa safari |
| 4. | Tani 11 hadi 22 | 5,000/= kwa safari |
| 5. | Zaidi ya tani 22 | 8,000/= kwa safari |

SEHEMU YA KUMI NA MBILI: ADA NA USHURU WA MGODI WA MADINI YA VIWANDANI

| Namba. | Madini | Ushuru au Ada ya Kibali kwa Mchimbaji (Shilingi) | Ushuru kwa Mnunuzi (Shilingi) |
|---|---|---|---|
| 1. | Gpsum | 50,000/= kwa kibali kwa mwaka | 10,000 kwa safari au tripu moja |
| 2. | Magnesite | 50,000/= kwa kibali kwa mwaka | 10,000 kwa safari au tripu moja |
| 3. | Felisper | 50,000/= kwa kibali kwa mwaka | 10,000 kwa safari au tripu moja |

SEHEMU YA KUMI NA TATU: ADA YA MAOMBI YA ZABUNI

| Namba. | Aina ya Huduma | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Maombi ya zabuni | 150,000/= |
| 2 | Zabuni za vizimba na maduka | 20,000/= |

SEHEMU YA KUMI NA NNE: ADA YA HUDUMA ZA KUMILIKI ARDHI

| Namba. | Matumizi ya Kiwanja | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Makazi | 500/= kwa kila mita ya mraba |
| 2. | Makazi na biashara | 500/= kwa kila mita ya mraba |
| 3. | Viwanda au Hoteli au Ghala au Biashara | 1,000/= kwa kila mita ya mraba |
| 4. | Huduma za kijamii (shule, Hospital) | 700/= kwa kila mita ya mraba |
| 5 | Kufufua mipaka ya kiwanja | 200,000/= |
| 6 | Malipo ya alama za upimaji | 10,000/= kila alama (beacon) |
| 7 | Kuonyeshwa kiwanja kwa mara nyingine | 50,000/= |
| 8 | Maombi ya kupatiwa (Site plan) | 10,000/= |
| 9 | Utafiti binafsi wa taarifa za kiwanja | 20,000/= |
| 10 | Kufanya uthamini kwa ajili ya kuhamisha miliki | 120,000/= kiwanja cha Makazi |
| | | 150,000/= kiwanja cha Makazi na Biashara |
| | | 200,000/= kiwanja cha Biashara |
| | | 1,000,000/= viwanda au taasisi |

SEHEMU YA KUMI NA TANO: USHURU WA MICHEZO YA KUBAHATISHA

| Namba. | Aina ya Huduma | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa mashine ya michezo ya kubahatisha | 50,000/= kwa kila mashine kwa kila mwezi-mlipaji ni mmiliki wa mashine |
| | | |

SEHEMU YA KUMI NA SITA (A): ADA YA KUENDESHA SHUGHULI ZA UTAMADUNI, BURUDANI NA MICHEZO

| Namba. | Aina ya Huduma | Kiwango cha Ada (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Kibali cha Dansi kutoka nje ya Halmashauri | 100,000/= kwa siku |
| 2. | Kibali cha Taarabu kutoka nje ya Halmashauri | 100,000/= kwa siku |
| 3. | Kibali cha sherehe za harusi ambazo hazifanyiki katika kumbi | 25,000/= kwa siku |
| 4. | Kibali cha Sherehe za harusi katika kumbi | 5% ya gharama iliyolipwa na mkodishaji |
| 5. | Kibali cha Disco/Dansi/Taarabu vikundi ndani ya Halmashauri | 20,000/= kwa siku |
| 6. | Kibali cha Sherehe za Camp za vijana | 10,000/= kwa siku |
| 7. | Kibali cha Maonesho ya muziki kwenye magari ya matangazo | 20,000/= kwa siku |
| 8. | Kibali cha Matangazo | 20,000/= kwa siku |
| 9. | Kibali cha kurekodi Filamu na Harusi katika Bustani na maeneo ya wazi na Kumbukumbu | 20,000/= |
| 10. | Kibali cha matambara ya burudani yanayofungwa katika maeneo mbalimbali ndani ya Halmashauri | 10,000/= kwa tambara kwa siku saba |
| 11. | Kibali cha kuweka Posters katika nguzo, miti, kuta mbalimbali | 300/= kwa poster, kwa siku |
| 12. | Kibali cha kufanya matamasha yanayofanyika katika maeneo mengine | 50,000/= kwa siku |
| 13. | Kibali cha kukodisha maeneo ya wazi kwa ajili ya mikutano ya dini | 20,000/= kwa siku |
| 14. | Kibali cha kuendesha mchezo wa “game” kwa kutumia TV | 180,000/= kwa Mwaka<br>15,000/= kwa mwezi |
| 15 | Ada ya kiingilio kwenye viwanja vya michezo | 3% ya kiingilio |

SEHEMU YA KUMI NA SITA (B)

FOMU YA MAOMBI YA KIBALI CHA KUENDESHA SHUGHULI ZA UTAMADUNI, BURUDANI NA MICHEZO

SEHEMU YA KWANZA (Taarifa za Mwombaji)

| | |
|---|---|
| 1. Jina la Mwombaji au Kampuni;..…………… | 2. Anwani ya Mwombaji;………..……… |
| 3. Aina ya Shughuli; ……………..……..... | 4. Eneo analokusudia kufanya shughuli……… |
| 5. Muda wa kuanza; ………………………… | 6. Muda wa kumaliza ……………………………… |
| 7. Ada ya kibali Shilingi.…………………........... | 8. Stakabadhi ya malipo; …………………… |
| Saini: …………………………. Tarehe: …………………….. | |

SEHEMU YA PILI (Kwa Matumizi ya Ofisi)

| | |
|---|---|
| 1. Maombi Na.…………….……..… | 2. Ada ya kibali Sh:. ………….......... |
| 3. Namba ya Stakabadhi ya malipo: ……….. | 4. Tarehe:…………………………….. |
| | |

Maoni ya Afisa Mwidhiniwa: - *Nakubali/Sikubali (*weka alama ya tiki kwa inayohusika*)
Sababu: ……………………………..……………………………………………
Jina: ………………………… Saini: …………………………………
Tarehe:………. Mwezi................. Mwaka..................................................

SEHEMU YA KUMI NA SABA: USHURU WA MAZAO YA UVUVI

| Namba | Aina ya Huduma | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Minada ya samaki katika mwalo au eneo maalum la kuuzia | Asilimia Tano (5%) ya bei ya mazao |
| 2. | Ushuru wa mazao ya uvuvi bila ya kutumia mnada | |
| | i. Gunia la dagaa wakavu kwa vipimo vifuatavyo: | |
| | (a) Chini ya kilo 50 | 5,000 kwa gunia |
| | (b) Kuanzia kilo 51 hadi kilo 100 | 10,000 kwa gunia |
| | (c) Kuanzia kilo 101 | 15,000 kwa gunia |

| | | |
|---|---|---|
| | ii) Samaki wabichi | 1000/= ndoo ndogo na 2000 kwa ndoo kubwa |

SEHEMU YA KUMI NA NANE
KIBALI CHA KUTUMIA SOKO

1. Jina la mwombaji na anuani yake…………………..................…
2. Kibali cha…………………..………………….............................
3. Eneo ambalo kibali hicho kitatumika……………………………
4. Muda wa kibali ni kuanzia tarehe...hadi tarehe.…..saa…………
5. Masharti ya kutumia kibali hicho ni pamoja na:
(a)………………………………........
(b)……………………………………
(c)………………………………..
6. Tarehe ya kikao iliyoidhinisha kibali……........................................
Muhtasari Namba.............
Imesainiwa na:

Jina……………………………………  Na.……………………………

………………………  …………………………..

Sahihi ya Mkuu wa Soko  Sahihi ya mwombaji

Tarehe…………………………  Tarehe…………………………..

Mhuri………………………………

USHURU WA KIZIMBA/MEZA KWENYE MASOKO YA ………...... NAMBA .............

| Namba | Aina ya Huduma | Kiwango cha Kodi kwa Mwezi au Siku (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Kizimba | 5,000/= kwa mwezi |
| 2. | Kizimba vya muda mfupi | 1,000/= kwa siku |
| 3. | Kodi ya duka au kioski au kibanda | 20,000/= kwa mwezi |
| 4. | Kodi ya stoo na Ofisi | 50,000/= hadi 1,000,000/= kwa mwezi |
| 5 | Kodi ya maghala | 300,000/= hadi 1,000,000/= kwa mwezi |

USHURU WA MAGARI YA MIZIGO KWENYE MASOKO, MINADA NA MAGULIO

| Namba. | | Aina za Mazao | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|---|

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | A. Ushuru wa Gunia | |
| 1. | | Vitunguu | 1000 kwa kila gunia au roba |
| 2. | | Viazi mbatata | 1000 kwa kila gunia au roba |
| 3. | | Karanga | 1000 kwa gunia au roba |
| 4. | | Nazi | 1000 kwa gunia au roba |
| | | B. Ushuru wa Matenga | |
| 1. | | Maembe | 2000/= kwa kila tenga |
| 2. | | Papai | 2000/=kwa kila tenga |
| 3. | | Nyanya | 2000/= kwa kila tenga |
| 4. | | Ndizi | 500/= kwa kila Mkungu |
| 5. | | Samaki wakavu | 3000/= kwa kila tenga |
| | | Samaki wabichi | 2000/= kwa kila ndoo kubwa |
| 6. | | Samaki wabichi | 1000/= kwa kila ndoo ndogo |
| | | C. Ushuru wa Kiroba | |
| 1. | | Nyanya chungu | 2000/= kwa kila kiroba |
| 2. | | Pilipili | 2000/= kwa kila kiroba |
| 3. | | Karoti | 2000/= kwa kila kiroba |
| 4. | | Matango | 2000/= kwa kila kiroba |
| 5. | | Ndimu | 2000/= kwa kila kiroba |
| 6. | | Limau | 2000/= kwa kila kiroba |
| 7. | | Pesheni | 2000/= kwa kila kiroba |
| 9. | | Parachichi | 2000/= kwa kila kiroba |
| 10, | | Peasi | 2000/= kwa kila kiroba |
| 11. | | Embe | 2000/= kwa kila gunia/roba |
| 12. | | Machungwa | 2000/= kwa kila gunia/roba |
| Namba. | | Aina za Mazao | Kiwango cha Ushuru |
| 1. | | Viazi vitamu | 1000/= kwa kila gunia au roba |
| 2. | | Mihogo | 1000/= kwa kila gunia au roba |
| 3. | | Kunde | 1000/= kwa kila gunia au roba |
| 4. | | Njegere | 1000/= kwa kila gunia au roba |
| 5. | | Choroko, mbatata, magimbi | 1000/= kwa kila gunia au roba |
| | | | |
| 1. | | Ushuru wa bidhaa zisizo katika | 10,000 kwa tani moja |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | magunia au kiroba au tenga au box | |

SEHEMU YA KUMI NA TISA: USHURU WA MAGARI YA MIZIGO KWENYE VITUO VYA MABASI NA MAEGESHO

| Namba | Aina ya Gari | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Gari lolote la mizigo | 5,000/= Kwa siku |

USHURU WA VYOMBO VYA USAFIRI KITUONI

| Namba. | Aina ya Chombo | Kiwango cha Ushuru (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Basi Dogo la abiria kati ya 1 hadi 20 | 2,000/= kwa siku |
| 2. | Basi kubwa la abiria kati ya 20 hadi 28 | 3,000/=kwa siku |
| 3. | Basi kubwa la abiria 28 na kuendelea | 5,000/= kwa siku |
| 4. | Gari Dogo (Teksi) | 1,000/= kwa siku |
| 5. | Gari Dogo (Binafsi) | 500/= kwa siku |
| 6. | Magari ya Mizigo (Pick-up) | 1,200/= kwa siku |
| 7. | Pikipiki (Bodaboda) | 500/= kwa siku |
| 8. | Bajaji | 1,000/= kwa siku |
| 9. | Magari mengine | 1,000/= kwasiku |
| 10. | Ada ya Kuingia mtu mmoja | 200/= kila anapoingia |

KULAZA CHOMBOCHA USAFIRI KITUO MAALUM

| Namba. | Aina ya Chombo | Ushuru wa kulaza chombo cha usafiri (Shilingi) |
|---|---|---|
| 1. | Basi kubwa la abiria kati ya 20-28 | 4,000/= kwa siku |
| 2. | Basi kubwa la abiria 28 na kuendelea | 5,000/= kwa siku |
| 3. | Basi Dogo la abiria kati ya 1-20 | 3,000/= kwa siku |
| 4. | Gari Dogo (Teksi) | 3,000/= kwa siku |
| 5. | Gari Dogo (Binafsi) | 1,000/= kwa siku |
| 6. | Malori na Tela zaidi ya tani 3 | 5000/= kwa siku |
| 7. | Malori na Tela tani 3 na zaidi | 3,000/= kwa siku |
| 8. | Magari ya Mizigo (Pick-up) | 3,000/= kwa siku |
| 9. | Magari mengine | 3,000/= kwa siku |
| 10. | Pikipiki | 1,000/= kwa siku |

GHARAMA ZA USAJILI WA TEKSI

| Namba. | Aina ya Chombo | Ada ya Usajili kwa Mwaka (Shilingi) |
| --- | --- | --- |
| 1. | Teksi | 60,000/= |

JEDWALI LA PILI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 14)*

HATI YA KUKIRI NA KUFIFILISHA KOSA

Mimi ……………………………………………………… nakiri KWA HIARI YANGU MWENYEWE mbele ya …………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe, kwamba mnamo tarehe …… ya mwezi ……. mwaka …… nilitenda kosa la kukiuka masharti ya aya ya …… ya Sheria Ndogo ya Ada na Ushuru ya Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe ya mwaka, 2023.

Kwa Mamlaka aliyopewa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe, niko tayari kulipa kiasi cha Ada au Ushuru ninaodaiwa pamoja na faini badala ya kushtakiwa Mahakamani.

NATHIBITISHA KWAMBA MAELEZO HAPO JUU NI YA KWELI NA NIMEYATOA MIMI MWENYEWE KWA HIARI YANGU KADRI YA UFAHAMU WANGU

Leo tarehe…………. ya Mwezi…………..… Mwaka …………….

Jina……………………………….. Saini………………………

MBELE YANGU:

Jina: …………………………………..……………………

Saini………………………..……………………….………

Wadhifa: …………………………………………………………

Tarehe…………………………………………………

Lakiri ya Halmashauri ya Wilaya Korogwe imegongwa kwenye sheria Ndogo hii kufutia azimio lililopitishwa katika Mkutano wa Baraza la Madiwani la Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe uliofanyika Tarehe 5/11/2021 na Kushudiwa na Lakiri hiyo ikigongwa mbele ya :-

GOODLUCK A. MWANGOMANGO
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe*

KALLAGHE S. YUSUPH
*Mwenyekiti*

*Halmashauri ya Wilaya ya Korogwe*

NAKUBALI,

Dodoma,
31 Oktoba, 2023

MOHAMED OMARI MCHENGERWA (MB)
*Waziri wa Nchi – Ofisi ya Rais,*
*(Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa)*